



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO



TAREHE: 06 JULAI, 2023

## TAARIFA KWA UMMA

### KUKANUSHA TAARIFA YA UWEPO WA HARUFU MBAYA STENDI YA MABASI YA MAGUFULI

Kufuatia taarifa ya Uongo iliyoripotiwa na mtandao wa Jamii forums tarehe 4 Julai, 2023 yenye kichwa cha habari "Harufu mbaya ndani ya stendi ya mabasi ya Magufuli yawa kero kubwa kwa wasafiri"

Taarifa hiyo inaeleza kuwa harufu hiyo inatokea kwenye chemba katika eneo wanaposimama abiria wanaosubiri basi la Happy Nation au jirani na yanaposimama mabasi ya Abood.

Manispaa inakanusha taarifa hiyo na inawaomba wasafiri na umma kwa ujumla kuipuuza taarifa hiyo kwasababu haina ukweli wowote na eneo hilo ni eneo ambalo lina abiria muda wote na hakujawahi kutolewa malalamiko na watumiaji wake kuwa kuna changamoto ya harufu mbaya.

Aidha, Manispaa imeendelea kuśimamia usafi wa mazingira na ujenzi wa miundombinu ndani ya kituo ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi bila kero au usumbufu wa aina yoyote.

**Ubungo Yetu Fahari Yetu**